## Mbinu za kufanikiwa biashara mtandao

mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali

# MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.mjasriamari.co.tz/ ISSN 3456-1679. Na. 12, Jumatano Januari 29, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100

### HUKU RAIS SAMIA AKINENA...

# Azimio la Dar laikomboa Afrika

"Ili kufanikisha azma hiyo ndani ya muda wa miaka mitano ijayo, tutahitaji uwekezaji wenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 13, ambapo dola bilioni 5 zitapatikana kutoka sekta binafsi hapa nchini," amesema Rais Samia.

- Lengo ni kufikia watu milioni 300 ndani ya bara hili




## Unayopaswa kufanya kama mjasiriamali

## Kanuni muhimu unapofuga kuku wa kienyeji

# Azimio la Dar laikomboa Afrika

NA MWANDISHI WETU

**AFRIKA imejikomboa yenyewe kuhusu suala la nishati, baada ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika Kuhusu Nishati kuhitimishwa jana, huku wakuu waliohudhuria wakitia saini 'Azimio la Dar' litakalowezesha Waafrika milioni 300 kufikishiwa huduma ya umeme ifikapo mwaka 2030.**



Mkutano wa wakuu wa nchi na viongozi wengine, ulimalizika jana lakini juzi ulitanguliwa na mawaziri wa kisekta kabla ya viongozi hao kuhitimisha.

Akizungumza katika mkutano huo jana, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Tanzania ni moja kati ya nchi 12 zitakazozindua mpango mahususi wa kitaifa kuhusu nishati.

Kupitia mpango huo unatarajiwa kuongeza kasi ya kuunganisha umeme nchini hadi kufikia asilimia 72 ifikapo mwaka 2030.

"Ili kufanikisha azma hiyo ndani ya muda wa miaka mitano ijayo, tutahitaji uwekezaji wenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 13, ambapo dola bilioni 5 zitapatikana kutoka sekta binafsi hapa nchini," amesema Rais Samia.

Awali katika siku ya kwanza ya mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alisema baada ya kupata uhuru, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao.

"Inasikitisha kwamba idadi ya Waafrika ambao hawana umeme inakadiriwa kuwa milioni 571. kutokana na hali hii, Mkutano huu uliitishwa, ukiwa na lengo kubwa lakini linaloweza kufikiwa la kuongeza upatikanaji wa umeme kwa angalau watu milioni 300 barani Afrika katika miaka mitano ijayo

"Kama ilivyobainishwa katika Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), leo (juzi) Dar es Salaam inayo heshima ya kuwa mwenyeji wa wajumbe kutoka Afrika na kwingineko, wakihudhuria Mkutano huu muhimu unaolenga kuimarisha azma ya Afrika ya kuipatia bara hili nishati.

"Baada ya kupata Uhuru mwaka 1960, nchi za Afrika zimepiga hatua kubwa katika kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi wao. Tanzania ilikuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 21 pekee wakati wa Uhuru, kwa sasa nchi ina uwezo wa kuzalisha megawati 3,160."

Akiwa ameibeba ajenda ya nishati salama mkononi mwake, Rais Dk. Samia amevunja na kuandika rekodi ya aina yake kwa kuwa Rais wa kwanza nchini aliyewahi kupokea idadi kubwa ya wakuu wa nchi 25 kujai kwa pamoja nchini.

Nchi ambao wakuu wake wamethibitisha kushiriki ni Algeria, Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan, Malawi, Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

# Wafanyabiashara walia utitiri wa Kodi

NA MWANDISHI WETU

**KUTOKANA na uwepo wa utitiri wa kodi,serikali imeombwa kutazama upya sharia za kodi ili kuzifanya ziwe rafiki na zinazolipika, hivyo kuwafanya wafanyabiashara wawe waaminifu kulipa badala ya kukwepa.**

Wafanyabiashara hao waliiomba serikali kutazama haswa kodi ambazo zinawakandamiza ikiwemo ile ya ushuru wa huduma (Service Levy) ambao unatozwa kwenye halmashauri mbalimbali nchini ili kuondoa usumbufu uliopo.

Wafanyabiashara hao waliamua kutema nyongo, mbele ya Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Balozi Ombeni Sefue wakati alipokutana na wafanyabiashara hao Jijini Arusha.

Mwenyekiti wa Chama cha Wataalam wa Kodi Tanzania Kanda ya Kaskazini, Nicholas Duhia alisema, wamewasilisha maoni yao kwa tume lakini kubwa zaidi ni kuhusu sheria za Kodi inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) lakini pia kodi ya huduma ishuke kutoka asilimia 3 hadi kufika 0.1 kulingana na huduma walizotoa.

"Kila halmshauri inamalipo yake katika ulipaji wa ushuru wa huduma hii ni kero lakini wamiliki wa hoteli wameongezewa kodi ya huduma ya takataka wakati magari ya kuzoa taka ni machache hivyo kodi hizi ziwekwe katika dirisha moja ili walipaji walipe kodi kwa kiwango kidogo na si kodi kubwa zaidi huku mhusika wa biashara husika hanufaiki na biashara yake"

Juliana Donald kutoka Umoja wa Wafanyabiashara Wanawake Arusha ameomba TRA kuacha kuweka vizuizi vya kodi kwani linaleta usumbufu kwa kuzuia magari yenye mizigo kuendelea na safari zake badala ya kudai mhusika wa mzigo kuwa



# Mpango aishukuru IMF kuiunga Tanzania

NA MWANDISHI WETU

**MAKAMU wa Rais Dkt. Philip Mpango jana amekutana na kufanya mazungumzo na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Bo Li, mazungumzo yaliyofanyika kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.**

Katika mazungumzo hayo, Dkt. Philip Mpango ameishukuru IMF kwa kuendelea kuiunga mkono Tanzania kupitia programu mbalimbali ikiwemo dirisha la mikopo nafuu ya nyongeza ya kuchochea kasi ya kuimarisha uchumi baada ya Janga la UVIKO-19 na misukosuko itokanayo na vita pamoja na programu ya kuimarisha uwezo wa nchi kukabiliana changamoto zitokanazo na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Amesema kupitia programu hizo, zimechangia ukuaji wa uchumi, kudhibiti mfumuko wa bei na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi.

Kwa upande wake Bo Li ameipongeza Tanzania kwa kuimarisha uchumi na kufanikisha utekelezaji wa programu za ushirikiano ikiwamo programu kupitia ECF na RSF. Aidha ameipongeza Tanzania kwa kutekeleza vyema programu ya ECF na kupata alama za juu katika tathimini ya nne.

Aidha, Li aameipongeza Tanzania kwa kuwa nchi ya mfano iliyochaguliwa pamoja na Madagascar kutekeleza mpango kabambe wa utafutaji wa fedha za mazingira kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwamo sekta binafsi, washirika wa maendeleo na AZAKI.

# Ulinzi wa mfumo wa ikolojia baharini wahimizwa

NA MWANDISHI WETU

**NCHI za Ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi zimetakiwa kushirikiana katika kulinda mifumo ikolojia inayotegemea afya ya bahari na ukanda wa pwani.**

Wito huo umetolewa na Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais Christina Mndeme wakati akifungua Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi ya Mazingira juzi jijini Dar es Salaam.

Amesema mkutano huo unaoshirikisha nchi wanachama ambazo ni Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Shelisheli, Re-Union, Afrika Kusini na Tanzania, unaashiria hatua kubwa ya maendeleo katika kuhakikisha ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali za Bahari ya Hindi vinakuwepo.

Mndeme amesema Tanzania inajivunia kuwa Mwenyekiti wa Mkataba wa Nairobi na imejitoa kikamilifu katika kuendeleza malengo ya mkataba huu kwa manufaa ya mazingira ya bahari katika Ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi (WIO).

Ameahidi kuwa Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kufanya kazi pamoja na Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi katika kufikia mafanikio yaliyooneshwa katika Mpango wa Kazi (2025-2028) na Maamuzi ya COP 11.

Aidha, Mndeme amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake thabiti ya kuwezesha hifadhi ya mazingira ya bahirini na kuendelea kuunga mkono katika utekelezaji wa programu ya kazi na Maamuzi ya COP 11.

"Chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia tumepiga hatua kubwa katika ulinzi wa mazingira, hasa kupitia uhamasishaji wa vyanzo vya nishati safi na endelevu," amesema.

Mkutano huo unaotarajiwa kufungwa Januari 31, 2025 umewakutanisha wataalamu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, maafisa viungo wa kitaifa wa Mkataba wa Nairobi, mashirika na taasisi za kitafiti.

## Mhandisi Manala ataja faida za Kongomano la Nishati

NA PAUL KAYANDA, Kahama



**KONGAMANO la Nishati la Afrika lililofanyika nchini Tanzania juzi na jana, linatoa fursa muhimu kwa nchi yetu na bara zima katika kuimarisha ajenda ya maendeleo endelevu kupitia upatikanaji wa nishati safi na ya uhakika.**

Licha ya Tanzania kuwa na rasilimali kubwa za kuzalisha umeme wa jua na upepo, bado tunategemea vyanzo vya nishati visivyo endelevu kama mafuta na kuni, jambo linalohitaji mabadiliko ya haraka.

Mhandisi aliyebobea katika nishati, Manala Tabu Mbumba alisema kuwa Afrika imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za nishati jadidifu, kama vile jua, upepo, na maji. Hata hivyo, uwekezaji katika sekta hii bado ni mdogo, hali inayohitaji juhudi za kushirikiana kikanda na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika teknolojia za nishati safi.

Mhandisi Manala aligusia changamoto kubwa ya upatikanaji wa nishati vijijini, akisema kuwa zaidi ya asilimia 50 ya watu barani Afrika hawana umeme, na sehemu kubwa ya watu hao ni kutoka vijijini.

Alisisitiza umuhimu wa kutumia teknolojia ya mini-grids na off-grid inayotumia vyanzo vya nishati jadidifu ili kuwafikia wananchi wa vijijini kwa bei nafuu.

Pia, alizungumzia umuhimu wa ushirikiano wa kikanda katika miradi ya nishati, akisisitiza kwamba miradi kama mabomba ya gesi, usambazaji wa umeme wa kikanda, na sera zinazowezesha biashara ya nishati baina ya nchi zitasaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza upatikanaji wa nishati.

Kwa upande mwingine, Mhandisi Manala alisisitiza haja ya kuwekeza katika teknolojia za kisasa na kukuza wataalamu wa ndani katika sekta ya nishati.

# MAONI

## Kwa mikakati hii, Afrika itafikia lengo

**MKUTANO wa M300 uliojadili nishati Afrika ulimalizika jana, huku kukiwa na ahadi za kila aina ikiwemo ile ya Rais wa Benki ya Asia Infrastructure Investment Bank (AIIB), Jin Liqun aliahidi benki hiyo itatoa Dola Bilioni 1.5 kuunga mkono upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 Afrika ifikapo 2030.**

Ahadi hiyo ameitoa ikiwa siku ya kwanza ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika unaoendelea Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika unaendelea ukiwa ukiwa umebeba ajenda kuu ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa wakazi wote wa bara hili.

Mkutano huo uliopewa jina la Mission 300 (M300) unaongozwa na kaulimbiu inayosema: 'Kuharakisha upatikanaji wa Nishati Afrika', ukiwa na malengo ya kujadili dhana nzima ya upatikanaji wa umeme kwa wote hususan katika nyakati ambazo viongozi wa Afrika wanasisitiza matumizi ya nishati safi na salama.

Tanzania itanufaika na mkutano huo hasa ikizingatiwa kuwa wakuu wa mataifa hayo wataidhinisha Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, ambao wakuu hao wanakubaliana kufanya mageuzi yatakayosaidia kufikia lengo la upatikanaji wa nishati kwa wote kwa njia za kuaminika, nafuu na endelevu.

Takwimu za nishati kwa Afrika zinaonesha kuwa hadi mwaka 2022 asilimia 83 ya watu milioni 685 walikuwa hawajafikiwa na nishati hiyo. Kwa msingi huo, mkutano huo unadhamiria kuhimiza kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali, ikiwemo kuingia makubaliano ili umeme uwafikie watu milioni 300 ifikapo mwaka 2030.

Katika mkutano huo wenye azma ya kuwafikia watu hao milioni 300, nchi 14 zitasaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika Awamu ya Kwanza.

Nchi hizo ni Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Tunapenda kuipongeza benki hiyo kutokana na msaada mkubwa ambao umeamua kuutoa kwa Afrika, ikiwa ni kusaidia kupatikana kwa umeme barani humu.




# FIKRA YA MJASIRIAMALI

## 'Mchongo' utakaokusaidia ukipokea vifaranga vya kuku

NA MWANDISHI MAALUM

**MARA nyingi ufugaji wa kuku huanza na vifaranga, na kwa kuwa vifaranga huweza kuathirika haraka na mazingira, maandalizi mazuri kabla hawajaletwa ni muhimu sana.**

Vifaranga wakiwa na umri wa juma moja huhitaji eneo la sentimeta za mraba 65 kila mmoja au mete moja ya mraba kwa vifaranga 120 hadi 150.

Kabla hujaingiza vifaranga safisha banda lako vizuri ndani na nje pamoja na mazingira yake. Pakikauka paka chokaa kwenye kuta zote. Hakikisha banda limekuwa tupu kwa wiki moja au mbili baada ya kusafishwa. Tandaza maranda bandani kisha juu yake weka magazeti au "chick papers".

Hakikisha una idadi ya kutosha ya vyombo vya chakula na maji kulingana na idadi ya kuku. Pia uwe na chakula bora cha kuanzishia.

Tayarisha chanzo cha joto angalau kwa saa 3 - 5 kabla vifaranga havijaingia ili joto la nyuzi joto 33 - 35 lipatikane.

Ukishawaleta vifaranga

Hesabu na kukagua vifaranga wakati wa kuweka bandani. Changanya maji safi na "glucose" pamoja na dawa za kuanzishia kisha wapatie. Dawa hii wapatie kwa siku 3 hadi 5 kulingana na maelezo ya dawa utakayotumia. Wapatie chakula baada ya saa 2 - 3 toka walipowasili na kunywa maji yenye "glucose" na dawa za kuanzishia.

Tumia kitabu kutunza kumbukumbu ya idadi, tarehe, aina ya vifaranga na chakula, kampuni ya vifaranga, magonjwa na matibabu yake, madawa yaliyotumika na kinga, na vifo toka siku ya mwanzo hadi wakati wa kuuza.

Kumbuka vifaranga wanatakiwa wapewe chakula bora na salama kwa ajili ya kuchochea ukuaji na kinga dhidi ya magongwa. Chakula kilicholowa na chenye ukungu kisitumike kabisa.

Ila wakati ukishawapokea ni lazima utayarishe mahali pa kulelea kwa kutumia vifaa mbalimbali kama vile, 'hard board' kwa ajili ya uzio mviringo, uzio wa eneo la meta moja ya mraba hutosha kulea vifaranga 100 – 150 hadi watakapokuwa na umri wa wiki mbili. Uongezwe kadri vifaranga wanavyoongezeka umri au ukubwa. Uzio uwe na vitundu kwa ajili ya kupitisha hewa.

Pia kuna maranda au nyasi zilizokatwakatwa au magunzi yaliyopondwa kwa ajili ya kufunika sakafu: Hunyonya unyevunyevu na kufanya banda liwe kavu, huleta joto(hutunza joto), hukausha na kuua vijidudu viletavyo magonjwa. Badilisha maranda yaliyolowana.

Kileta joto (source of heat): Unaweza infra red bulb, bulb za kawaida, taa ya chemli au jiko la mkaa kwa ajili ya kuleta joto na mwanga. Kileta joto ni vema kiwekwe katikati ya uzio ili pande zote zipate joto la kulingana. Kileta joto kiongezwe au kipunguzwe joto kufuatana na mahitaji ya vifaranga.

Kuna siku tutajimwaga zaidi na kuzungumza kw akina juu ya hili na kukusaidia wewe mjasiriamali unayetaka kufuga kuku.



# Zanzibar kujenga mfumo wa ununuzi wa umma

NA MWANDISHI WETU

**NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande ametoa wito kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzaber kujenga Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa kutumia wataalam wa ndani ili kusimamia kikamilifu fedha za Serikali zinazotumika katika ununuzi.**

Alitoa wito huo jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyotembelea Mamlaka ya Ununuzi wa Umma nchini (PPRA) kwa ajili ya kujifunza masuala ya ununuzi wa umma kwa ujumla.

Alisema Mfumo huo pia utasaidia kurahisisha mchakato wa ununuzi pamoja na kuongeza uwazi wa zabuni kwa kujua thamani halisi ya fedha.

Aidha Chande aliipongeza kamati hiyo kwa kufanya uamuzi wa kuja kujifunza PPRA katika kipindi hiki ili kwenda kuboresha Muswada wa Sheria ya Ununuzi ambao utajadiliwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

"Haya ni maamuzi sahihi kwa sababu Taasisi za Umma ndio ambazo zinatumia bajeti kubwa katika ununzi wa umma kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti zetu zinakwenda kwenye ununuzi, kwa hiyo tunapoenda kupitisha Mswada wetu tuhakikishe Sheria imewekwa vizuri ili kuepuka changamoto", aliongeza Chande.

Aliwakaribisha kutembelea PPRA mara kwa mara kwa ajili ya kuendelea kujifunza zaidi na ikiwezekana waende jijini Arusha ambako kumesimikwa Mfumo wa Ununuzi ili waone uhalisia uliopo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mwanaasha Khamis Juma alisema kwa sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya maboresho ya Sheria ya Ununuzi, hivyo kamati imeamua kuja kujifunza ili waweze kuishauri Serikali kikamilifu.

"Kama nilivyosema hapo awali, hii ni Kamati ya Bayeti na kazi yeke ni kupitisha Bajeti ya Serikali ambayo ndani yake kuna miradi na kwenye miradi kuna ununuzi, kwa hiyo tumeamua tuje tuone wenzetu wanafanyaje, Sheria zao zikoje, ili tuone namna bora ya kuishauri Serikali", aliongeza Mwanaasha.

Naye Naibu Waziri wa Ofisi ya Raisi, Fedha na Mipango, Zanzibar, Mhe. Juma Makungu Juma, alisema wamekuja kujifunza kwa sababu fedha nyingi za Taifa zinatumika katika ununuzi hivyo ni muhimu Serikali ihakikishe fedha hizo zinatumika vizuri.

Alisema kuwa wamekuja kuchukua uzoefu wa taratibu mbalimbali za ununuzi pamja na mafanikio kwa sababu taratibu hizo za zinatofautiana kati ya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kujadili mafanikio na changamoto zilizopo katika masuala ya ununuzi.

# Kigoma watakiwa kujitokeza msaada wa kisheria ya Mama Samia

NA MWANDISHI WETU, Kigoma

**NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Amon Mpanju amesema Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ni moja ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto.**

Mpango wa MTAKUWWA- 2023/24-2028/29 unaohimiza kupambana na mila na desturi zenye madhara ambazo zikiendekezwa zinasababisha kukiukwa kwa haki za wanawake, watoto na makundi maalum.

Mpanju amesema hayo mkoani Kigoma wakati akitoa salamu katika uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Suluhu Hassan ambapo Mgeni Rasmi alikuwa ni Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Damas Ndumbaro.

Akizindua Kampeni hiyo Dkt. Ndumbaro amesema Kampeni ya Msaada wa Kisheria itatekelezwa kwa muda wa siku tisa katika Halmashauri tisa za Mkoa wa Kigoma na kuwafikia Wananchi katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha matatizo yote ya Kisheria yanapatiwa suluhu.

# Wa kufich a fedha nyumbani

NA MWANDISHI WETU

**WANANCHI wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro wametakiwa kutumia huduma rasmi za fedha kutunza fedha zao badala ya kutunza nyumbani ili ziweze kuingia katika mzunguko wa fedha na kuongezeka thamani.**

Rai hiyo imetolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Hussein Urughu, alipokuwa akifungua mafunzo ya elimu ya fedha, wakati timu ya maafisa kutoka Wizara ya Fedha iliyoambatana na maafisa kutoka taasisi na watoa huduma za fedha ilipowasili kwa ajili ya kutoa elimu ya fedha na kuhamasisha utumiaji wa huduma za fedha zilizo rasmi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Alisema kuwa njia ya kutunza fedha nyumbani si salama kutokana na kuweza kupata hasara kutokana na majanga ya moto au kuibiwa na hivyo kushauri wananchi kutumia huduma za benki kutunza fedha ili ziingie katika mzunguko watu wapate mikopo ili kukuza uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

''Watu wanauza mifugo wanakaa na fedha nyumbani ambapo wangeweza kuweka sehemu nyingine ikazaa faida, wengine wanaingia vikundi vya kukopeshana bila kufuata taratibu na baadaye wanadhulumiwa, hivyo ni matarajio yetu kuwa elimu ya fedha mtakayoitoa itawafungua wananchi kuondokana na changamoto hizo," alisema Urughu.

Alisema kuwa masuala ya fedha yanafanyika kimazoea katika jamii kwani sheria kanuni na taratibu za fedha hazifuatwi hivyo elimu ya fedha ni chachu kwa wananchi wa Ngorongoro kupata uelewa wa namna bora ya kutunza na kutumia fedha zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Aidha, alisema kuwa elimu ya fedha itawasaidia wananchi kuweza kujua namna ya kuweka akiba, umuhimu wa bima, jinsi ya kuwekeza pamoja na kujipanga vema kutumia fursa za mikopo inayotolea na Halmashauri ili kuweza kujikwamua kiuchumi.

Naye Afisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, alieleza kuwa ni muhimu kila mwananchi kuhakikisha kuwa wanachukua mkopo katika taasisi za fedha zilizosajiliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

# Mbinu za kufanikiwa biashara mtandao

NA MWANDISHI MAALUM

**BIASHARA ya mtandao ni mfumo wa biashara ambao unamlipa mwanachama aliyejiunga na kampuni husika kutokana na mauzo yake binafsi na mauzo ya wanachama ambao mwanachama huyo aliwashawishi wajiunge na biashara ya kampuni hiyo. Katika ukurasa huu, tutajifunza jinsi ya kupata mafanikio katika biashara hizi za mtandao.**

Biashara ya mtandao inatoa fursa kwa mwanachama kupata malipo endelevu bila ya yeye kujihusisha katika mauzo. Malipo endelevu ni malipo ambayo mwanachama anapata kutokana na kazi aliyoifanya mara moja na akaendelea kupata malipo muda mrefu baadaye bila yeye mwenyewe kuhusika moja kwa moja. Mfano ni pale mwanachama anapomwingiza mwanachama mgeni katika kampuni fulani na mwanachama huyu mgeni akanunua bidhaa iitwayo X.

Huyu mwanachama mgeni akiipenda bidhaa hii na akatoa oda ya kuipata kila mwezi, mwanachama aliyemwingiza mgeni huyu ataendelea kulipwa bonasi inayotokana na mauzo ya bidhaa hiyo mwezi ule alipomwingiza mgeni huyu na ataendelea kulipwa kila mwezi baadaye ili mradi mwanachama huyu mgeni anaendelea kutumia bidhaa X.

Ulipwaji wa bonasi hii bila wewe kujishughulisha tena unakupa kipato bila wewe kufanya kazi tena. Ukiwa umeweza kuwasajili chini yako wanachama wengi wa namna hii, basi tayari utapata kipato endelevu kikubwa kila mwezi.

Biashara ya mtandao inakupa pia fursa ya kupata kipato kutokana na vizazi mbalimbali chini yako. Wale wanachama uliowasajili wewe na kuwafundisha jinsi ya kufanya kazi, ni kizazi chako cha kwanza.

Wanachama wa kizazi chako cha kwanza nao watawasajili ndugu zao, rafiki zao na watu wengine na kuwaelekeza jinsi ya kufanya mauzo ya bidhaa za kampuni yenu. Vivyo hivyo, hawa waliosajiliwa na wale uliowasajili, watawasajili ndugu, jamaa na rafiki zao. Kwa mtindo huu, utakuwa umejijengea mtandao wa watu chini yako wanaofanya biashara ya kampuni yako.

Hii ndiyo maana ya biashara ya mtandao. Wale waliosajiliwa na wanachama wa kizazi chako cha kwanza, watakuwa wanachama wa kizazi chako cha pili na hivyo kuendelea na vizazi vingi chini yako.

Kampuni itakulipa kutokana na mauzo yanayofanywa wanachama wa vizazi vilivyo chini yako. Kila kampuni ina utaratibu wake kuhusu idadi ya vizazi vilivyo chini yako vitakavyolipwa. Kampuni nyingine, hazina ukomo wa idadi ya vizazi vilivyo chini yako vitakavyokupa malipo.

Biashara ya mtandao inakulipa kutokana na kazi ya wanachama uliowasili wewe binafsi na wanachama waliosajiliwa na wale uliowasajili na vizazi vilivyo chini yako. Hapa unapewa kipato kutokana na mwendelezo wa nguvu zako za kusajili na mwendelezo wa maelekezo uliyoyatoa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine (leveraged income).

### Ili Kufanikiwa katika Biashara Ya Mtandao Fanya Yafuatayo

Awali ya yote inabidi nieleze na kutoa mkazo kuwa biashara za mtandao ni kufanya kazi na watu na kuwafundisha jinsi ya kubadilika na kupata kipato kufikia viwango vya juu.

Kitu kikubwa ni kujifunza na kutumia mbinu bora za kujenga timu chini yako. Ukisha kuwa na



kikosi ambacho umekifundisha vizuri, kitafanya kazi na kukufanya uongeze kipato chako kila mwezi.

Unaanza na kuwafundisha wale ambao umewasajili wewe binafsi, nao watawafundisha waliowasajili na zoezi hilo kujirudiarudia na hatimaye kupata kikosi bora kinachofanya kazi. Kampuni nyingi za mtandao zinatoa mafunzo na kutoa nyenzo za kusaidia katika kutoa mafunzo.

Sasa ili uweze kupata mafanikio kwenye biashara za mtandao, pitia kwa makini na tekeleza yafuatayo:

### Chagua Vizuri Kampuni Yako Ya Mtandao

Kwangu mimi binafsi, hili ni la maana kuliko mengine yote ambayo tutayajadili hapa chini kwa sababu ikiwa utaangukia mikononi mwa kampuni mbovu, haya yote tunayoyajadili kwenye mada hii hayatakusaidia, hata kama utatumia nguvu na mbinu za namna gani. Zingatia yafuatayo katika kuchagua kampuni yako ya kufanya nayo biashara:

Sifa Za Kampuni: Chunguza sifa za mmiliki wa kampuni unayotaka kujiunga nayo na historia ya kampuni kwa ujumla. Jee, kampuni ina anwani ya kudumu? Kampuni iliyo kwenye biashara hii kwa muda mrefu, itakuwa na uhakika zaidi katika shughuli zake.

Chunguza vile vile katika kipindi ambacho kampuni imekuwa ikifanya kazi imekuwa na rekodi gani. Jee, imewaingiza wanachama kwenye migogoro ya aina yo yote? Kuna wanachama ambao wametajirika na kampuni hiyo? Inakua kibiashaara, imefikia ukomo au inateremka kibiashara? Jiunge kwenye kampuni ambayo majibu yake kwa maswali hayo ni mazuri.

**2**. Ubora Wa Bidhaa Au Huduma Za Kampuni: Mteja ye yote yule atanunua bidhaa ya kampuni au atapenda kupata huduma za kampuni pale tu ambapo amepata sifa kuwa bidhaa za kampuni hiyo au huduma ya kampuni hiyo itamsaidia kuondoa matatizo aliyo nayo na si kinyume cha hilo. Kampuni yenye bidhaa nzuri au huduma nzuri itakupunguzia kazi ya kufanya matangazo au kutoa maelezo badala yake utapata wateja wengi walioelekezwa kwako (referrals) na kupata faida kubwa.

**3.** Mpango Mzuri Wa Malipo: Mpango wa malipo wa kampuni unayofanya nayo kazi ndio utakaosema wewe kama mwanachama utapata kiasi gani kutokana na kazi uliyoifanya. Kwa vile ulijiunga ili upate kipato kizuri, haina maana kujiunga na kampuni ambayo haina mpango mzuri wa malipo. Ni vizuri kujiunga na kampuni ambayo ina mpango wa malipo unaoeleweka kiurahisi, unaotekelezeka na unaolipa vizuri.

**4**. Msaada Wa Mafunzo Na Nyenzo Za Kazi: Kampuni inayotoa mafunzo ya bure kwa wanachama wake, vipeperushi na vifaa vingine vya kusaidia kufanya kazi itakusaidia kufikia malengo yako ya kupata kipato kikubwa kwa muda mfupi zaidi.

Kampuni iliyo bora itatoa njia nyingi za kutoa msaada, namna nyingi za kuweza kujifunza kuhusu biashara yake, mabango, tovuti binafsi na vitu vingine ili uweze kupanda kiurahisi na kufikia malengo yako.

### Ielewe Vizuri Kampuni Yako

Chukua muda wa kutosha kujifunza kuhusu mpango wa malipo wa kampuni yako, kampuni nyingine zina vitu vingi sana ambavyo ungeweza kuvifanya.

Ukisha pata undani wa kampuni, amua njia yako utakayoifuata katika kufikia malengo yako katika biashara ya kampuni hiyo. Pata ushauri kila mara kutoka kwa watu walio juu yako ili ujue njia walizozitumia kufanikiwa katika biashara ya kampuni hiyo.

### Ongoza Timu Yako Vizuri

Wanachama wapya kwenye kampuni wanahitaji msaada kama vile ulivyohitaji wewe wakati unaanza biashara na kampuni hiyo. Hakikisha unatoa muda wa kutosha kuwafundisha kuhusu biashara yenu, washike mkono hadi pale watakapoanza kumudu kuifanya biasharaa hiyo wenyewe. Kumbuka kuwa kufanikiwa kwa walio chini yako ndiyo mafanikio yako. Kusajili wanachama chini yako kisha kuwaacha yatima hakutakusogeza po pote katika biashara yako.

### Tumia Vizuri Mtandao

Kwa wakati tulio nao sasa, hakuna chombo bora cha kufanyia matangazo ya biashara yako zaidi ya matumizi ya mtandao (internet). Unaweza kutumia mitandao ya kijamii (social media sites), ukajenga blog au tovuti kwa ajili ya kuitangaza biashara unayoifanya.

Mitandao ya kijamii yote mikubwa – Facebook, Google+, Instagram, Tweeter na mingineyo inaruhusu watu kufungua akaunti bure na kutangaza biashara zao bure kabisa. Baadhi ya mitandao inaruhusu kufungua kurasa za kibiashara, kwa mfano, Fan Page kwenye facebook, ambamo utajenga urafiki na watu mbalimbali ambao wataelewa ni biashara gani unaifanya.

### Panga Muda Wa Kujiendeleza

Mafanikio katika biashara ya mtandao yameonekana kuendana na ukuaji wa kiwango chako wewe binafsi kifikra na kiutendaji.

Uchu wa kujifunza, kujiendeleza binafsi na kukua binafsi.

Hapo juu ndilo neno kuu katika kipengele hiki cha kukusaidia kukua kibiashara. Watu wote waliofikia mafanikio makubwa walisikiliza kanda za kaseti, walisoma vitabu na walihudhuria semina. Walitenga kipande cha siku kwa ajili ya kujiendeleza binafsi, Na, inaonekana kuwa, kadiri walivyopata mafanikio zaidi -ndivyo walivyotenga muda zaidi kwa ajili ya kujiendeleza.

Imebainishwa kuwa kama unataka kufika kiwango fulani, au kulifikia lengo fulani -lazima ufikie kuwa ni aina ya mtu ambaye amefikia kiwango hicho au amefikia lengo hilo. Vipawa vimejificha ndani yako, vikingojea kuamshwa. Unachotakiwa kukifanya ni kuviibua.

Chagua watu wachache waliofanikiwa katika biashara hii na sikiliza mikanda yao ya video au soma vitabu walivyoviandika. Mimi napenda kuwasikiliza na kusoma vitabu vya Jim Rohn, Eric Worre na Randy Gage.



# Unayopaswa kufanya kama mjasiriamali

NA MWANDISHI MAALUM

**LAZIMA tutambue kuwa, ujasiriamali ni muhimu zaidi kwetu kuliko tunavyofikiri. Wengi wetu tunatambua kwamba ardhi, nguvukazi na mtaji vinahitajika kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma ambazo hudumisha na kuboresha maisha yetu. Lakini ujasiriamali ni njia isiyoonekana ya uzalishaji.**



Ardhi, nguvukazi na mtaji havizalishi chochote hadi pale vinapoingizwa katika matumizi yake. Vinahitaji kuelekezwa na kujikita katika matumizi yake kupitia akili fulani ya mwanadamu, akili ya kijasiriamali ambayo inatambua jinsi gani vinaweza kutumiwa kutengeneza thamani.

Mapokeo ya uchumi yaliasisi njia kuu nne za uzalishaji: ardhi, nguvukazi, mtaji, na ujasiriamali. Kwa kupitia kasoro kadhaa chache, njia ya mwisho ilitoweka, pamoja na mambo yake maridhawa, kutoka kwenye nadharia ya kiuchumi wakati fulani mwanzoni mwa karne ya 20.

Ukweli ni kwamba, ujasiriamali hautiliwi maanani sana kiasi kwamba hata dhana yake inaonekana kuwa ya juzijuzi. Neno ujasiriamali' lina mzizi wake kutoka kwenye neno la Kifaransa karne ya kumi na tatu, ambalo maana yake ni kufanya kitu fulani.

Hadi kufikia 16 lilitumika kumaanisha watu waliofanya biashara. Lakini ilikuwa ni hadi mwaka 1730 pale mchumi Richard Cantillon alipolitumia kumaanisha mtu ambaye alichukua hatari ya kifedha katika kuendesha biashara.

MSINGI WA UJASIRIAMALI

Mwaka 1803 pale ambapo mchumi wa Kifaransa Jean-Baptiste Say alipoelekezea dhima ya msingi ya wajasiriamali katika kutafuta matumizi zalishi zaidi ya rasilimali.

Madoido zaidi kwenye wazo hili yalifanyika mwaka 1848, pale

ambapo mwanafalsafa na mchumi wa Kiingereza anayeitwa John Stuart Mill alipowatambulisha wajasiriamali kama watu ambao wanachukua hatari katika usimamizi wa biashara.

Leo hii, wachumi wanaitazama dhima ya wajasiriamali kama wavumbuzi au katika kung'amua fursa au kuchukua hatari katika dunia yenye mustakabali usiotabirika na majaribio ya kufafanua zaidi dhana hii yanaendelea.

Uvumbuzi na ukuaji wa kiuchumi

Hakuna kipengele chochote cha ujasiriamali ambacho ni muhimu zaidi kwenye maendeleo ya mwanadamu na ukuaji wa kiuchumi kuliko uvumbuzi.

Maendeleo na ukuaji siyo tu ni matokeo ya kutumika zaidi kwa njia zinazoonekana za uzalishaji bali kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya uvumbuzi katika kufanya shughuli ya kiuchumi ya mwanadamu kuwa zalishi zaidi.

Katika uchumi shindani, wajasiriamali hukabiliana na msukumo usiokoma wa kuvumbua pale wanapohaha kutafuta njia za kuokoa zaidi gharama katika kutengeneza bidhaa bora zaidi, zinazopatikana kwa bei nafuu, kwa haraka zaidi, na usafi zaidi, ambazo ni za kisasa na zenye kuwavutia wateja. (Hebu fikiria maendeleo ya teknolojia kwenye simu au magari, kwa mfano, na mapinduzi katika namna ambayo vinatengenezwa).

Msukumo usiokoma wa kuinua uwezo zalishi kutafuta michakato yenye tija zaidi na bidhaa zenye ufanisi zaidi unadhihirisha ongezeko la juu katika viwango vyetu vya maisha.

Ukweli ni kwamba, tukirejea katika miaka ya 1950, mchumi wa Kimarekani na mshindi wa Tuzo ya Nobel anayeitwa Robert Solow alikokotoa kwamba asilimia 87 dhahiri ya ukuaji wa kiuchumi ulitokana na uvumbuzi. Hata hivyo

mwandishi wa sayansi wa Kiingereza anayeitwa Matt Ridley anaamini idadi hiyo inaweza hata kuwa ya juu zaidi leo hii.

SABABU ZA KUZINGATIA UJASIRIAMALI

kwa kuwa malighafi mpya, mashine mpya na mbinu zenye tija zaidi hutuwezesha kutumia muda mfupi na rasilimali chache katika kufanya ugavi wa mahitaji na matakwa yetu.

Uvumbuzi siyo tu unatengeneza bidhaa bora zaidi, bali unatengeneza pia rasilimali mpya, anasema mtaalamu wa Kimarekani wa usimamizi wa biashara anayeitwa Peter Drucker. Wajasiriamali hubadilisha vitu visivyo na thamani kama mchanga kuwa vyenye thamani kama vibanzi vya silikoni vya kompyuta. Na matokeo yake hizo rasilimali mpya zinaweza kutumika kutengeneza hata bidhaa za thamani kubwa zaidi, kama vile simu za kisasa za mkononi, maroboti na magari yanayojiendesha bila dereva.

Lakini uvumbuzi hauonekani tu kwenye vifaa vipya. Uvumbuzi, anasema Ridley, ni msawazishaji mkubwa. Leo hii, watu kwenye nchi maskini kabisa wana simu za mkononi zinazofanya kazi vizuri kama ilivyo kwenye nchi yoyote tajiri sana. Uvumbuzi ndiyo sababu ya kupungua kwa kasi kwa idadi ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri, na ndiyo sababu ya hali kuendelea kuwa hivyo.

Uvumbuzi, kwa maana hiyo huboresha maisha yetu; na kuna kiunganishi chenye nguvu baina ya uvumbuzi na idadi ya biashara mpya zinazoanzishwa. Idadi kubwa ya viwanda vinavyokua kwa kasi (kama vile vya teknolojia ya habari na mawasiliano, uhalisia wa kutengeneza, michakato ya viwandani ya kibaiolojia, huduma ya afya kupitia teknolojia ya mawasiliano na programu za huduma za kifedha) inaonesha ni kampuni changa zinazokua, na siyo kampuni za zamani zilizojizatiti.

Kwa hakika, makampuni makubwa, kupitia rasilimali zao za mtaji na wafanyakazi yanaweza pia kuwa ya kijasiriamali: kumbuka Walkman kutoka Kampuni ya Sony.

Hata hivyo, ni kampuni mpya, ndogo zaidi, na zinazochipukia ambazo ndizo zenye kuhusika zaidi na uvumbuzi, na kiasi kikubwa cha utengenezaji wa ajira mpya.

# Wakulima wanawake Kahama wanavyopigwa tafu uchumi wa kilimo

NA PAUL KAYANDA, Kahama

**KAMPUNI ya DORFLA yenye makao makuu yake katika Manispaa ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga, imeendelea kuwa msaada mkubwa kwa wanawake wakulima wa Manispaa hiyo kwa kuwapa zana bora za kilimo pamoja na kuwapatia elimu kuhusu kilimo cha kisasa.**

Huu ni mpango wa kimkakati ambao umelenga kuboresha uzalishaji wa kilimo, kuhakikisha mazao mengi yanapatikana, na kutoa fursa kwa wanawake ili kuboresha uchumi wao kupitia kilimo.

Hafla hiyo ilifanyika Januari 14,2025 ambayo wakulima wengi pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali, ambapo vifaa vilivyokabidhiwa ni pamoja na majembe ya kukokotwa na wanyama,(Plau,) na zana nyingine za kilimo.

DORFLA ilianzisha mpango maalum wa kuwawezesha wanawake wakulima wa Kahama kwa kutoa majembe hayo kwaajili ya kilimo bora, kwakutumua ng'ombe na punda, pamoja na vifaa vingine vya kisasa vya kilimo.

Lengo kuu la kampuni hii ni kuongeza tija ya uzalishaji na kusaidia wanawake kuwa na uhuru wa kifedha kupitia kilimo.

Kupitia mradi huu, wanawake wengi wameshuhudia mabadiliko makubwa katika maisha yao. Hii ni kutokana na ongezeko la mazao, kupungua kwa gharama za uzalishaji, na kuboreshwa kwa ubora wa mazao.

Zaidi ya hayo, DORFLA imeweza kushirikiana na serikali ya Manispaa ya Kahama na taasisi nyingine za maendeleo, akiwemo Mbunge wa Jimbo la Kahama, Jumanne Kishimba, ili kuhakikisha kwamba programu hii inaendelea kwa mafanikio na inafikia malengo yake ya muda mrefu.

Mmoja wa wanawake walionufaika na mpango huu ni Amina Hassan, mkulima kutoka kata ya Ngogwa ambaye anasema, "Kwa muda mrefu, tulikuwa tukitumia zana za zamani na kilimo tunashinda tunalima mpunga majarubani kutokana na zana duni, lakini baada ya DORFLA kutuletea majembe bora,ya ayotumika na ng'ombe sasa tumeweza kuongeza uzalishaji wetu mara mbili."

Vilevile, wanawake hawa wamejengewa uwezo wa kuanzisha vikundi vya kilimo, ambapo wanashirikiana katika usimamizi wa shughuli zao na hata katika masoko ya bidhaa zao. Kwa mfano, kuna vikundi vya wakulima wa mbogamboga na nafaka ambavyo vimeanzishwa kupitia msaada wa DORFLA, na kwa sasa wanapata masoko bora ya kuuza mazao yao, huku wakiendelea kupata elimu ya usimamizi wa biashara.

Viongozi wa Manispaa ya Kahama wamesema kuwa mradi huu wa DORFLA umeleta mabadiliko chanya katika jamii, hasa kwa wanawake ambao zamani walikuwa wakikumbwa na changamoto nyingi za kiuchumi. Hali hii inatoa motisha kwa serikali na mashirika mengine ya maendeleo kuwekeza zaidi katika miradi inayowafaidi wanawake, hasa kupitia kilimo.

kampuni ya DORFLA imethibitisha kuwa ni nguzo muhimu katika kuboresha maisha ya wanawake wakulima wa Manispaa ya Kahama. Kwa msaada huu wa kivitendo na elimu, wanawake hawa sasa wana uwezo wa kufanya kilimo cha kisasa na kuleta mabadiliko makubwa katika familia zao na jamii kwa ujumla.



Betha Mabula, ni Mkurugenzi wa kampuni ya DORFLA Trading Co. Ltd., inayojishughulisha na usindikaji wa mazao mbalimbali, ikiwemo zao kuu la mpunga, anasema kuwa kampuni yake kwa kushirikiana na wahisani, hususan shirika la MEDA la Marekani, hivi karibuni walifanya mafunzo ya kilimo cha kisasa cha mpunga.

"Lengo ni kuwaelekeza wakulima kuhusu kilimo cha kisasa, ili waweze kulima kidogo lakini kuvuna mavuno mengi," anasema Mabula.

Mabula anafafanua umuhimu wa jembe la ng'ombe katika kilimo, akisema kuwa ni chombo rahisi kutumia na kinachorahisisha shughli za kilimo. "Jembe la ng'ombe linatoa fursa kwa kila mtu, hata wale wasio na uwezo mkubwa wa kifedha, kutekeleza shughuli za kilimo kwa ufanisi. Linaleta mabadiliko makubwa katika uzalishaji, kwani lina uwezo wa kulima eneo kubwa kwa wakati mfupi," anasema Mabula.



Kampuni ya DORFLA inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mpango huu ili kuhakikisha kuwa vifaa hivyo vinatumika ipasavyo kuwasaidia wakulima kwa kulima kilimo bora na kuweza kupata mazao mengi. "Majembe haya yataboresha maisha ya wanawake kwa kulima kilimo bora cha mpunga. Tumegawia wanawake kila mmoja binafsi, badala ya vikundi, ili kuwawezesha kupandisha uchumi wao," anasema Mabula.

Mkurugenzi huyo anasisitiza kuwa kampuni yake imejikita zaidi katika kusaidia wanawake kwa sababu wanahitaji maendeleo na mradi huu ulianzishwa kwa nia ya kuwafaidi wanawake wa Manispaa ya Kahama. "Mwito wetu ni kwamba mafunzo haya na vifaa vitumike kwa ufanisi na kuleta mabadiliko chanya kwa wakulima wanawake," anasisitiza Mabula.

Pendo Matulanya, Mkuu wa Divisheni ya Kilimo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, alitumia nafasi hiyo kuwataka wakulima kutumia zana za kisasa kwa malengo yaliyo wazi. "Kwa sasa mmepewa vifaa bora, na ni jukumu lenu kuhakikisha mnatumia zana hizi kwa kilimo chenye tija. Vilevile, majembe haya yasiyauzwe, bali yatumike katika shughuli maalumu ya kilimo," alisema Matulanya.

Mbunge wa Jimbo la Kahama mjini, Jumanne Kibela Kishimba, akizungumza kwenye hafla ya ugawaji wa majembe ya ng'ombe iliyofanyika eneo la shule ya Msingi Mbulu Kata ya Mhongolo, alisisitiza umuhimu wa kuchanganya mazao mbalimbali ili wakulima waweze kupata mazao mengi.

Mbunge Kishimba alisema kuwa hicho kilicho fanywa na kampuni ni juhudi za kukuza sekta ya kilimo katika jimbo lake.

Kishimba alieleza kuwa msaada huu umejumuisha zana muhimu ambazo zitawawezesha wakulima kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

Alisema kuwa zana hizo ni muhimu kwa wakulima wa Manispaa ya Kahama, ambao wengi wao hutegemea kilimo cha mazao mbalimbali kama vile mahindi, mpunga na maharage.

Alifafanua ushirikiano wake na kampuni ya DORFLA ambayo imetowa msaada huu, ni hatua muhimu katika kuunga mkono wakulima na kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo.

Alisema kuwa, kupitia msaada huu, wakulima wataweza kupunguza matumizi ya nguvu kazi ya kimwili, kuboresha ubora wa mazao yao na hatimaye kuongeza mapato yao.

Kwa upande wake,kaimu mkurugenzi mtendaji kampuni ya Dolph, alisisitiza kuwa lengo la kampuni hiyo ni kuhakikisha kuwa wakulima wanapata zana bora za kilimo ili kuwasaidia katika kuongeza ufanisi na tija katika kazi zao.

Aidha Aliongeza kuwa kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na jamii na Serikali katika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata msaada unaohitajika ili kuendeleza shughuli zao za kilimo.

"Mimi ndiye niliyeshawishi kampuni ya DORFLA kuwapatia mafunzo na majembe haya, kwani wanawake wa Manispaa ya Kahama wanahitaji msaada mkubwa katika kilimo," alisema Kishimba.

### Wanufaika wa Mradi huu

Mary Kadushi pamoja na wanufaika wengine wamesema kuwa kabla ya mpango huu walikuwa wanatumia majembe ya mkono, lakini sasa wanatumia majembe ya mifugo kama ng'ombe na punda, na wanatarajia kupata mavuno mengi. "Kwa kutumia majembe haya, tunaamini tutaongeza tija na kupata mazao mengi," wamesema wanufaika.

Kwa kumalizia, DORFLA imekuwa nguzo muhimu katika kuboresha maisha ya wanawake wakulima wa Manispaa ya Kahama. Kwa msaada wa vifaa vya kisasa na elimu, wanawake hawa sasa wana uwezo wa kufanya kilimo cha kisasa na kuboresha maisha yao na ya jamii kwa ujumla.



# Kanuni muhimu unapofuga kuku wa kienyeji



NA MWANDISHI MAALUM

**WAKATI unapoamua kufuga kuku wa kienyeji, kuna kanuni bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji ni muhimu kwa kuongeza uzalishaji na kuhakikisha faida nzuri kwa mfugaji.**

Kuku wa kienyeji wanahitaji utunzaji wa kipekee kutokana na mazingira yao asili na changamoto za ufugaji wa kienyeji. Hapa kuna baadhi ya kanuni bora za kufuata katika ufugaji wa kuku wa kienyeji:

## Uchaguzi wa Kuku wa Kienyeji Bora

Kuchagua kuku bora kwa ajili ya ufugaji ni hatua muhimu kwa mafanikio ya mradi wako wa ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Kuku wenye sifa nzuri watakua haraka, watatoa mayai kwa wingi, na watakuwa na afya bora.

Kuku wa Kiafrika: Kuku wa kienyeji wanaozaliwa katika mazingira ya Kiafrika wana uwezo mzuri wa kuhimili magonjwa na hali ngumu ya mazingira.

Vifaranga Bora: Vifaranga wanapaswa kuchaguliwa kwa kuzingatia afya zao, nguvu, na uwezo wa kukua haraka.

## Utunzaji wa Mabanda

Banda bora ni muhimu ili kuwapa kuku wa kienyeji makazi salama na mazuri.

Mabanda yanapaswa kujengwa kwa ubora ili kulinda kuku dhidi ya hali mbaya ya hewa, wanyama wanaokula kuku na magonjwa.

Banda lenye hewa safi: Hakikisha kuna mzunguko mzuri wa hewa ndani ya banda ili kuepusha vumbi na joto kupita kiasi.

Safi na Salama: Mabanda yanapaswa kusafishwa mara kwa mara ili kuzuia magonjwa. Vyombo vya chakula na maji pia viwe safi.

Kinga Dhidi ya Wanyama Waharibifu: Weka uzio au miti ya kuzuia wanyama kama mbwa, paka, na ndege wakubwa kuwavamia kuku.

## Lishe Bora kwa Kuku

Lishe ni moja ya mambo muhimu katika ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Ingawa kuku wa kienyeji wanajulikana kwa uwezo wao wa kujitafutia chakula, bado ni muhimu kuwapa chakula cha ziada chenye virutubisho kamili.

Chakula cha Asili: Kuku wa kienyeji wanaweza kutafuta wadudu, mbegu, na mimea kwa ajili ya chakula. Ni vyema kuwaachia huru wakatafute chakula asilia kwa afya bora.

Mchanganyiko wa Nafaka: Wape mchanganyiko wa nafaka kama mahindi, mtama, na mpunga ambao unaongeza virutubisho muhimu kwa ukuaji wa kuku na uzalishaji wa mayai.

Vyakula vya Protini: Ongeza vyakula vya protini kama dagaa, mabaki ya nyama, na mabaki ya mboga kwa kuku ili kuboresha afya na uzalishaji wa mayai.

## Utunzaji wa Afya na Chanjo

Utunzaji mzuri wa afya ya kuku wa kienyeji husaidia kupunguza vifo na kuzuia magonjwa.

Kuku wa kienyeji wanapaswa kupewa chanjo na matibabu mara kwa mara ili kulinda dhidi ya magonjwa yanayoathiri uzalishaji.

Chanjo: Chanjo za kuku wa kienyeji zinasaidia kuzuia magonjwa kama mdondo (Newcastle Disease), homa ya kuku, na ndui. Ni muhimu kuwapa chanjo vifaranga kuanzia wiki za kwanza baada ya kuzaliwa.

Dawa za Minyoo na Vidudu: Hakikisha unawapa kuku dawa za minyoo na za kuua viroboto mara kwa mara ili kuhakikisha wanaendelea kuwa na afya bora.

Maji Safi: Hakikisha maji wanayokunywa ni safi na yenye afya ili kuzuia magonjwa ya tumbo yanayotokana na maji machafu.

## Kuzalisha Kuku

Mbinu za kuzalisha kuku wa kienyeji zinaweza kuendeshwa kwa njia ya asili au kutumia incubator za kisasa.

Hata hivyo, kuku wa kienyeji wana uwezo mzuri wa kuatamia mayai na kuzalisha vifaranga bila msaada wa mashine.

Kuatamia kwa Asili: Kuku jike mwenye afya nzuri anapaswa kuachiwa mayai kwa ajili ya kuatamia. Joto na mazingira salama ni muhimu kwa kuhakikisha vifaranga wanaanguliwa kwa wingi.

Udhibiti wa Mbuzi wa Kuku (Male): Hakikisha unakuwa na idadi nzuri ya mbuzi wa kuku kwa uwiano wa kuku jike ili kuongeza ubora wa mayai na uzalishaji wa vifaranga.

## Mzunguko wa Mayai

Ili kufanikisha uzalishaji endelevu wa kuku wa kienyeji, ni muhimu kuwa na mzunguko wa mayai.

Hii inahusisha kuvuna mayai kwa wakati na kuwatenga kuku wanaotaga mara kwa mara kwa ajili ya uzalishaji.

Kuhifadhi Mayai: Mayai yanayokusanywa kwa ajili ya kuuzwa au kuatamiwa yanapaswa kuhifadhiwa sehemu kavu, salama, na yenye baridi kidogo.

Usimamizi wa Uzalishaji: Weka kumbukumbu ya kuku wanaotaga ili kusaidia katika ufuatiliaji wa uzalishaji wa mayai na kuhakikisha unaendelea na uzalishaji mzuri wa vifaranga.

## Kupanga Ratiba

Ratiba nzuri ya kufuatilia uzalishaji wa kuku wa kienyeji ni muhimu kwa kupata faida.

Hakikisha unajua ni lini kuku wanapaswa kutaga, kuatamia, na kuuza kuku wazee ili kuweka mzunguko mzuri wa uzalishaji.

## Masoko na Mauzo

Ni muhimu kuwa na mpango wa masoko kabla ya kuanza ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Tafiti soko la ndani na nje ili kuhakikisha kwamba kuku na mayai yako yanapata wateja.

Masoko ya Jumla: Weka mahusiano mazuri na wauzaji wa jumla, migahawa, na watu binafsi wanaohitaji kuku wa kienyeji kwa wingi.

Masoko ya Rejareja: Unaweza kuuza kuku moja kwa moja kwa wateja wadogo kama familia na majirani.

## Faida na Gharama

Kwa kufuata kanuni hizi, unaweza kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza faida kwa urahisi.

Ufugaji wa kuku wa kienyeji unalipa vizuri hasa kwa kutegemea mazingira ya asili, na unahitaji uwekezaji mdogo ukilinganisha na kuku wa kisasa.



# Pambana na kilimo cha mbogamboga

**TUNAENDELEA kukuimarisha zaidi katika mambo haya, ambapo tutazungumzia kwa kina kilimo cha bustani ya mbogamboga ni njia nzuri ya kuzalisha chakula chenye afya na lishe bora huku pia kikiwa chanzo kizuri cha kipato.**



Kumbuka mbogamboga ni mazao yanayolimwa kwa ajili ya matumizi ya chakula, hasa majani, shina, mizizi na matunda.

Tanzania ni moja ya nchi zenye mazingira yanayofaa kwa kilimo cha mbogamboga kutokana na hali yake ya hewa na upatikanaji wa ardhi yenye rutuba.

Makala hii inaeleza kwa kina jinsi ya kuendesha kilimo bora cha bustani ya mbogamboga kuanzia maandalizi ya shamba, upandaji, matunzo hadi mavuno.

### Uchaguzi wa Aina za Mbogamboga kwa Bustani

Kabla ya kuanza kilimo, ni muhimu kuchagua aina ya mbogamboga zinazofaa kulingana na mahitaji ya soko, hali ya hewa, na udongo wa eneo lako.

Mbogamboga zinazolimwa kwa wingi nchini Tanzania ni pamoja na mchicha, spinachi, kabeji, bamia, karoti, nyanya, pilipili hoho, bilinganya na vitunguu.

Aina hizi zinapendwa kwa soko la ndani na la nje kutokana na lishe bora inayotokana na mboga hizi.

### Maandalizi ya Shamba la Bustani

Uchaguzi wa Eneo ni kitu cha kwanza kabisa, kwani kilimo cha bustani ya mbogamboga kinaweza kufanyika kwenye eneo lolote lenye nafasi ya kutosha na hali nzuri ya udongo.

Hakikisha eneo lina mwanga wa jua wa kutosha, kwa sababu mboga nyingi zinahitaji mwanga wa moja kwa moja kwa angalau saa 6 hadi 8 kwa siku.

Pia aina ya udongo wenye rutuba nyingi unafaa zaidi kwa kilimo cha mbogamboga.

Udongo wa kichanga na mfinyanzi wenye rutuba nzuri ni bora kwa mboga hizi.

Udongo unapaswa kuwa na uwezo mzuri wa kupitisha maji ili kuepuka maji kusimama, ambayo yanaweza kuharibu mizizi ya mimea.

### Matayarisho ya Shamba

Shamba linapaswa kulimwa vizuri ili kuondoa magugu na kupunguza ugumu wa udongo.

Mbolea ya asili kama samadi au mboji inaweza kuongezwa ili kuboresha rutuba ya udongo.

Pia, hakikisha udongo una kiasi cha unyevu wa kutosha kabla ya kupanda mbegu au miche.

### Kupanda Mbogamboga

Msimu bora wa kupanda mbogamboga hutegemea aina ya mboga na hali ya hewa.

Mboga nyingi zinaweza kupandwa mwanzoni mwa msimu wa mvua au wakati wowote ambapo maji ya kutosha yanapatikana kwa umwagiliaji.

### Kupanda Mbegu au Miche

Baadhi ya mbogamboga hupandwa kwa kutumia mbegu moja kwa moja, wakati nyingine zinahitaji kupandwa kwenye vitalu na kuhamishiwa shambani baada ya miche kuwa tayari.

Nyanya: Mbegu huoteshwa kwanza kwenye vitalu na miche kuhamishiwa bustanini baada ya wiki 6.

Karoti: Mbegu hupandwa moja kwa moja kwenye udongo na huhitaji nafasi ndogo kati ya mimea.

### Nafasi ya Kupanda

Nafasi kati ya mistari na mimea ni muhimu ili kuruhusu mzunguko wa hewa na upatikanaji wa mwanga kwa mimea.

Mchicha na spinachi: Nafasi ya sentimeta 10 hadi 20 kati ya mimea.

Nyanya na pilipili hoho: Nafasi ya mita 1 kati ya mistari na sentimeta 60 kati ya mimea.

### Matunzo ya Bustani ya Mbogamboga

Mbogamboga zinahitaji maji mara kwa mara, hasa kipindi cha mwanzo cha ukuaji.

Umwagiliaji mara mbili kwa siku, asubuhi na jioni, ni muhimu, hasa kwenye maeneo yenye joto kali au wakati wa kiangazi.

Mimea kama nyanya na pilipili zinahitaji maji ya kutosha ili kuzuia magonjwa kama kuoza kwa matunda.

### Palizi

Palilia bustani mara kwa mara ili kuondoa magugu yanayoshindana na mimea yako kwa virutubisho na maji.

Palizi pia husaidia kuzuia magonjwa na kuondoa mazingira ya wadudu hatari.

### Mbolea ya Ziada

Mbolea ya ziada inapaswa kuongezwa mara kwa mara ili kuhakikisha mimea inapata virutubisho vya kutosha kwa ukuaji na utoaji wa mazao bora.

Mbolea za asili kama samadi ni nzuri zaidi kwa mbogamboga, kwani hazina kemikali zinazoweza kuathiri ubora wa mazao.

### Udhibiti wa Wadudu na Magonjwa

Wadudu na magonjwa ni changamoto kubwa katika kilimo cha mbogamboga.

Magonjwa kama ukungu wa majani, madoa ya majani, na wadudu kama vidukari na nzi wa matunda wanaweza kuathiri mavuno.

Ni muhimu kutumia dawa za kuulia wadudu na magonjwa, lakini kwa upole ili kuzuia kemikali nyingi kuingia kwenye mimea.

Vidukari: Wadudu hawa hushambulia mboga kama spinachi, mchicha, na kabeji. Dawa za asili zinaweza kutumika kuzuia.

Nzi wa matunda: Hushambulia mboga kama pilipili na nyanya. Unaweza kutumia mtego wa nzi au dawa maalum za wadudu.

### Kuvuna na Kuhifadhi Mbogamboga

Kila aina ya mbogamboga ina kipindi chake maalum cha kuvuna.

Hakikisha unavuna mboga zako kwa wakati unaofaa ili kuzuia kuharibika kwa mazao.

Mchicha na spinachi: Huvunwa kwa kukata majani yaliyokomaa.

Nyanya: Huvunwa pale zinapokuwa na rangi kamili, zikiwa bado ngumu kidogo ili zisiharibike haraka baada ya kuvunwa.

Karoti: Huvunwa baada ya mizizi kuwa mikubwa na yenye rangi ya machungwa.

### Kuhifadhi

Baada ya kuvuna, mazao yanapaswa kuhifadhiwa vizuri ili yaweze kudumu kwa muda mrefu.

Hifadhi mazao mahali penye baridi au kivuli ili kuepusha kuoza au kupoteza ubora.

Faida za Kilimo cha Bustani ya Mbogamboga

Kilimo cha mbogamboga kinaweza kuongeza kipato cha familia, hasa katika maeneo ya mijini ambako soko la mboga ni kubwa. Mazao kama nyanya, pilipili, na karoti yana bei nzuri sokoni na yanauzika haraka.

### Kuboresha Afya

Mboga ni chanzo bora cha vitamini, madini, na nyuzilishe, hivyo husaidia kuboresha afya ya familia kwa kutoa lishe bora.

Pia, bustani ya mbogamboga inaweza kusaidia kupunguza gharama za manunuzi ya chakula.

### Kulinda Mazingira

Bustani ya mbogamboga inaweza kusaidia kuboresha mazingira, hasa kwa kutumia mbinu za kilimo hai (organic farming), ambazo zinaepuka kemikali na kulinda afya ya udongo kwa muda mrefu.

### Hitimisho

Kilimo cha bustani ya mbogamboga ni shughuli yenye faida kwa familia na jamii nzima.

Kwa kufuata mbinu bora za kilimo, kuanzia maandalizi ya shamba, matunzo ya mimea, hadi mavuno, unaweza kufanikiwa kupata mazao bora na kuongeza kipato chako.

Bustani ya mbogamboga inahitaji uangalizi wa karibu, lakini faida zake ni kubwa sana, hususan katika kuboresha lishe na afya ya familia na kuchangia kipato.

# Kufuga samaki nyumbani kunavyolipa





**UFUGAJI wa samaki nyumbani ni njia rahisi na ya gharama nafuu ya kuzalisha chakula cha protini bora au kujipatia kipato.**

Njia hii inafaa kwa mtu yeyote mwenye nafasi ndogo au aliye na nia ya kuanzisha ufugaji wa samaki kwa kiwango kidogo kabla ya kupanua shughuli zake.

Kwa kufuata mwongozo huu, utaweza kufanikisha ufugaji wa samaki nyumbani kwa mafanikio.

**1. Chagua Aina ya Samaki wa Kufuga**

Samaki wanaofaa kufugwa nyumbani ni wale wanaokua haraka, wanaohimili mazingira rahisi, na wanaopendwa sokoni:

Sato (Tilapia) ni maarufu kwa ukuaji wa haraka na ladha nzuri, kambare (Catfish) nao ni rahisi kufuga na wanaostahimili mazingira magumu, pia kuna samaki wa mapambo kama vile goldfish na koi, kwa biashara ya mapambo.

**2. Tayarisha Eneo la Ufugaji**

Unahitaji eneo linalofaa kwa kuweka tanki au chombo cha kufugia samaki. Chagua sehemu yenye mazingira yafuatayo, kama vile mahali penye kivuli kidogo.

Epuka mwanga wa moja kwa moja wa jua, lakini hakikisha kuna mwanga wa kutosha na upatikanaji wa maji safi, yaani hakikisha una chanzo cha maji safi na salama kama kisima, maji ya bomba, au mvua na ukubwa wa nafasi eneo linapaswa kuwa na nafasi ya kutosha kwa tank au chombo kingine unachotumia.

**3. Aina ya Vifaa vya Kufugia Samaki**

Unaweza kutumia vifaa rahisi vinavyopatikana karibu na wewe:

Tank za Plastiki ni rahisi kuzipata na kusafirisha, mabati yaliyofunikwa na plastiki yanaweza kutumika kama chombo cha muda mrefu.

Mifuko maalum ya nailoni inafaa kwa ufugaji wa muda mfupi. Mapipa au Madumu Makubwa: Chaguo rahisi kwa kiwango kidogo cha samaki.

**Matayarisho ya Maji**

Ubora wa maji ni muhimu sana kwa afya na ukuaji wa samaki:

Usafi wa Maji: Tumia maji safi na ya kutibiwa kama inavyohitajika.

Oksijeni ya Kutosha: Weka pampu ya hewa (aerator) ili kuongeza oksijeni kwenye maji.

PH ya Maji: Hakikisha kiwango cha pH kipo kati ya 6.5 – 8.5, kulingana na aina ya samaki.

**Lishe ya Samaki**

Samaki wanahitaji lishe bora ili waweze kukua haraka:

Chakula cha Kiwandani: Protini ya kiwango cha juu inahitajika kwa ukuaji wa samaki.

Chakula cha Asili: Mabaki ya chakula, mabuu, na majani ya mimea yanaweza kutumika.

Ratiba ya Kulisha: Wape chakula mara mbili kwa siku kwa kiasi kinachotosha ili kuzuia uchafuzi wa maji.

**Utunzaji wa Mazingira ya Samaki**

Badilisha Maji Mara kwa Mara: Badilisha 20-30% ya maji kila baada ya siku 3-5 ili kudumisha usafi.

Usafi wa Tank: Safisha tank mara kwa mara ili kuondoa taka na mabaki ya chakula.

Kudhibiti Joto la Maji: Joto linapaswa kuwa kati ya nyuzi joto 25°C – 30°C kwa samaki wengi wa tropiki.

**Udhibiti wa Magonjwa**

Magonjwa yanaweza kusababisha hasara kubwa, hivyo yafuatayo ni muhimu:

Ukaguzi wa Mara kwa Mara: Chunguza samaki kwa dalili za magonjwa kama vile madoa, uvimbe, au harakati zisizo za kawaida.

Matibabu ya Magonjwa: Tumia dawa zinazofaa mara unapogundua dalili za ugonjwa.

Kuzuia Magonjwa: Hakikisha mazingira ya maji ni safi na samaki wanapewa chakula bora.

**Kuvuna Samaki**

Samaki wako watakuwa tayari kuvunwa baada ya miezi 4-6 kulingana na aina na hali ya ufugaji:

Mbinu za Kuvuna: Tumia nyavu ndogo kuvua samaki bila kuwaumiza.

Usindikaji: Baada ya kuvuna, safisha samaki na uwaandae kwa ajili ya matumizi au soko.

**Faida za Kufuga Samaki Nyumbani**

Gharama Nafuu: Inahitaji mtaji mdogo kuanza.

Kupunguza Upotevu wa Nafasi: Huwezi kuhitaji eneo kubwa.

Chakula Bora: Unapata samaki safi na wenye afya kwa matumizi ya familia.

Kipato cha Ziada: Unaweza kuuza samaki na kupata kipato.

**Hitimisho**

Ufugaji wa samaki nyumbani ni mradi rahisi na wenye faida kubwa ikiwa utafuata hatua na mbinu sahihi.

Kwa mazingira yanayofaa, lishe bora, na matunzo ya mara kwa mara, unaweza kufanikisha mradi huu na kuendeleza maisha yako kiuchumi na kiafya.



# Wanawake wajasiriamali, wanapolazimishwa kuisaka kausha damu

**TAKWIMU za usawa wa kijinsia katika ajira zinaonyesha kwamba kufikia mwaka wa 2014 Watanzania milioni 2.1 walikuwa wameajiriwa katika sekta rasmi, ikiwa ni pamoja na serekalini na sekta binafsi, kwa mujibu wa kituo cha taifa cha takwimu nchini humo.**

Hatahivyo takwimu rasmi za serikali zinaonyesha pia kwamba zaidi ya 60% ya wanawake walio kati ya umri wa miaka 18 hadi 24 yaani milioni 13.9 wanajishughulisha na shughuli zisizo rasmi yaani biashara ndogondogo na kilimo.

Hii maana yake ni kwamba ni asilimia 0.75 tu ya wanawake walioko katika umri wa kufanya kazi ndio wapo katika sekta rasmi. Kwa maneno mengine, idadi kubwa ya wanawake walioko katika umri wa kufanya kazi nchini Tanzania ni wajasiriamali.

Licha ya kuwa na idadi kubwa ya wanawake wenye ujasiri wa kubuni na kuendesha biashara, kasi ya ukuaji wa mitaji yao bado ni finyu.

Chanzo kikuu cha mitaji karibuni duniani kote ni mikopo rasmi ya kibiashara. Hata hivyo, tafiti zinaonesha kuwa wanawake wengi wajasiriamali kutoka nchi zinazoinukia ikiwemo Tanzania hawana mikopo kutoka benki na taasisi rasmi za kifedha.

Kwa miaka mingi, dhana iliyoaminika ni kuwa wanawake wengi hawapati mikopo sababu pesa hazitoshi, lakini takwimu zinapingana na dhana hiyo.

Utafiti uliochapishwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka 2014 unaonesha kuwa zaidi ya 80% ya maombi ya mikopo ilitengwa kwa ajili ya wajasiriamali wanawake na 90% iliiva kwa ajili ya kutolewa. Hatahivyo, ni 18% ya wanawake wajasiriamali ambao waliomba mikopo benki na 28% waliomba mikopo katika taasisi nyenginezo za kifedha.

Takwimu hizo zinaashiria kuwa tatizo si uwepo wa fedha za mikopo bali utayari wa wanawake wajasiriamali kukopa.

Moja ya wataalamu waliondaa utafiti huo Vanessa Naegels hivi karibuni ameandika katika jarida la The Conversation kuwa, utayari wa wanawake kuomba mikopo unaathiriwa na mambo makuu mawili, dhana hasi juu ya mikopo rasmi ya kifedha na kukatishwa tamaa.

Kwamujibu wa utafiti huo, wanawake wengi wamebainisha kuwa hawaamini kuwa wanabaguliwa na maafisa mikopo kwenye taasisi za kifedha.

Kilio cha waliowengi ni masharti yanayoambatana na mikopo hiyo ambayo yanakuwa kikwazo kwao. Sharti la kwanza lililolalamikiwa ni viwango vikubwa vya riba vinavyotozwa na mabenki kufikia 20% mpaka 30% kwa mwaka.

Wanawake hao pia wametaja kama dhamana ya mali kuwa ni kikwazo, wengi wao hawana mali kama nyumba au ardhi za kuweka rehani ili wapate mikopo.

Kwa wale ambao wenye mali hizo ni waume wamesema wenza wao hawawezi kuwapa ruhusa ya kuziweka rehani.

Kuna ambao wanamali zinazofaa kuwekwa rehani, lakini wamesema hawawezi kuzikopea wakiogopa kuzipoteza pale watakaposhindwa kulipa madeni yao.

Baadhi ya wajasiriamali wamelalamikia mchakato ni mrefu na wenye gharama. Kuna ambao wamelalamikia tabia za baadhi ya maafisa mikopo wakisema kuna ambao huwatongoza na kutaka wawape rushwa ya ngono ili wawasaidie.

Kutokuwa na ufahamu mzuri wa masuala ya kifedha na mikopo pia umetajwa kuwa ni kikwazo, wajasiriamali wengi wanawake wamesema hawakuwa wakijuwa kuwa wanapochelewa kulipa mikopo yao gharama za malipo huongezeka ama benki wana uwezo wa kuuza mali zao pale watakaposhindwa kulipa madeni kwa wakati .

Utafiti umeonesha kuwa kuna machungu ya aina mbili, ya moja kwa moja na ya kusikia kwa wengine. Hali zote mbili hizo zinachangia wanawake wajasiriamali kutoomba mikopo.

Baadhi ya wanawake waliohojiwa kwenye utafiti huo wamesema walishaomba mikopo huko nyuma na kukataliwa, wengine walipitia mashaka tele kwenye kulipa madeni yao na wengine kuombwa rushwa. Baadhi yao wamepata matatizo hayo kwenye mikopo isiyorasmi hali iliyopelekea kuwa na dhana hasi mpaka kwenye utayari wao kwenye kuomba mikopo rasmi.

Kwa kiasi kikubwa kuna ambao wamesikia habari za ugumu wa kupata na kurejesha mikopo kutoka kwa watu wengine ima wajasiriamali wenzao au habari zilizozagaa kwenye jamii.


Simulizi hizo huwafanya baadhi kutojaribu kabisa kuomba mikopo. Kuna ambao wanaamini wakiwa na mikopo watakosa uhuru wa kutumia pesa zao kwa namna wanavyoona inafaa.




Ni dhahiri kulingana na utafiti wa ILO kuwa si kweli kuwa wanawake wajasiriamali waliowengi hawapati mikopo sababu ya ufinyu wa pesa.

Tatizo si pesa, bali dhana hasi zilizoota mizizi mirefu juu ya mikopo ya kibiashara. Ili kujenga utayari wa wajsairiamali wanawake kukopa dhana hizo potofu inabidi ziondoshwe, lakini haitakuwa kazi nyepesi.

Kwamujibu wa watafiti, njia bora zaidi na yenye tija ni kutoa elimu mahususi ya masuala ya kifedha kwa wanawake wajasiriamali. Ni kupitia elimu pekee wajasiriamali wanawake wanaweza kutunza hesabu zao na kulinda mitaji yao na kuikuza kwa kupitia mikopo rasmi.



# KUMBE RICK ROSS MKWEPA KODI


LOS ANGELES, Marekani

**HATIMAYE rapa mwenye jina kubwa, Rick Ross, ameingia mikononi mwa mamlaka za ukusanyaji kodi za Jimbo la Georgia. Taarifa zaidi zinadai kuwa Ross alikwepa kodi ya Dola za Marekani 65,000 na hiyo ilitokea mwaka 2021.**

**Hata hivyo, hicho hakionekani kuwa ni kiasi kikubwa cha fedha kwa rapa huyo anayemiliki mjengo wenye vyumba 109, ambao miaka mingi iliyopita ilikuwa ukimilikiwa na bondia mkongwe, Evander Holyfie**

# SOULJA BOY AWA YUDA

LOS ANGELES, Marekani



**WAKATI fulani, Soulja Boy alikuwa sehemu ya marapa waliokuwa wakimponda Rais wa Marekani, Donald Trump.**

Hata hivyo, hivi karibuni Soulja Boy aliambatana na wenzake hao, wakiwamo Snoop Dog na Nelly, kwenda kutumbuiza katika sherehe ya kuapishwa kwa Trump.

Sasa, wakati huu mashabiki wake wakimponda na kumwita mnafiki, Soulja Boy ameibuka na kuwajibu kwamba alifuata pesa. "Nililipwa pesa ya maana," alisema rapa huyo.


# YA P. DIDDY BADO HAYAJATULIA

LOS ANGELES, Marekani

**FAMILIA moja imeibuka na kumshushia lawama nzito rapa anayesota gerezani kwa tuhuma za udhalilishaji wa kingono, P. Diddy.**


Kwa mujibu wa familia hiyo, Diddy hakuomba radhi baada ya moja ya sherehe zake kusababisha vifo vya ndugu zao mwaka 1991.

Tukio hilo ni la mwaka 1991, ambapo Diddy aliandaa mechi ya mchezo wa kikapu, sherehe ambayo ilimalizika kwa mamia ya watu kupoteza maisha kutokana na msongamano mkubwa.





# RASHFORD MBADALA WA NKUNKU



MANCHESTER, England

**MANCHESTER United huenda ikamnunua mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, kwa mkopo ikiwa Muingereza Marcus Rashford, 27, ataondoka katika klabu hiyo.**


Rashford yuko tayari kusubiri kupata uhamisho wa kwenda Barcelona, ambako mambo yanakwenda mwisho mwisho ili atue katika kikosi hicho.

# LEVERKUSEN WAMTAKA McATEE

LEVERKUSEN, Ujerumani


**BAYER Leverkusen wamefanya mawasiliano na Manchester City kuhusu uhamisho wa mkopo wa kiungo wa kati wa England chini ya umri wa miaka 21 James McAtee, 22.**

**Kocha wa City Pep Guardiola hatamzuia Mctee iwapo anataka kujiunga na mabingwa hao wa Ujerumani. Wakati huo, kiungo wa kati wa Argentina Emiliano Buendia, 28, yuko mbioni kujiunga na Leverkusen kutoka Aston Villa kwa mkopo.**



# VILLA WAMFUATILIA FAYTH

LONDON, England



TIMU ya Villa pia wako kwenye mazungumzo na mlinzi wa Villarreal mwenye umri wa miaka 27 na Argentina Juan Foyth.

Naye mshambuliaji wa Villa na Colombia Jhon Duran, 21, anasakwa kwa udi na uvumba na klabu ya Saudi Arabia Al-Nassr kwa Euro 100m wakati wanatafuta mshirika mpya wa Cristiano Ronaldo.

# KARIM AZUSHA VITA

LONDON, England

TIMU ya Liverpool na Chelsea wako tayari kuchuana na Napoli kwa ajili ya kumnunua fowadi wa Borussia Dortmund na Ujerumani Karim Adeyemi, 23, lakini wanaweza kusubiri hadi msimu wa joto kufanya uhamisho.

Nao Wolves wapo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa Lens na Austria yenye thamani ya £16m Kevin Danso, 26.



# MADRID, BAYERN WAPO KWA DEAN

MADRID, Hispania

Real Madrid, Bayern Munich na Juventus wanavutiwa na beki wa kimataifa wa Bournemouth chini ya umri wa miaka 21 Dean Huijsen.

Newcastle wanavutiwa na mlinzi wa kimataifa wa Ukraine wa Cherries, Illia Zabarnyi, 22, lakini wanajua kuwa dili halitawezekana hadi msimu wa joto.



Mjasiriamali spoti
MJASIRIAMALI JANUARI 29,2025

# CAF YAICHONGEA TANZANIA

NA ASHA SEKEFU

**TANZANIA imepangwa Kundi C katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025 zitakazofanyika kuanzia Desemba 21 mwaka huu hadi Januari 18 mwakani, 2026 pamoja na jirani zao, Uganda, Tunisia na Nigeria.**

Katika Droo ya upangaji makundi ya AFCON 2025 iliyofanyika juzi usiku katika Ukumbi wa Mohammed V National Theatre Jijini Raba nchini Morocco, wenyeji wa Fainali hizo wapo Kundi A pamoja na Mali, Zambia na Comoro, wakati mabingwa watetezi, Ivory Coast wapo Kundi F pamoja na Cameroon, Gabon na Msumbiji.

Kundi B linazikutanisha Misri, Afrika Kusini, Angola na Zimbabwe, wakati D kuja Senegal, DRC, Benin na Botswana na Kundi E wapo Algeria, Burkina Faso, Equatorial Guinea na Sudan.

MAKUNDI YOTE AFCON 2025 MOROCCO
KUNDI A: Morocco, Mali, Zambia, Comoro
KUNDI B: Misri, Afrika Kusini , Angola, Zimbabwe
KUNDI C: Nigeria, Tunisia, Uganda, Tanzania
KUNDI D: Senegal, DRC, Benin, Botswana
KUNDI E: Algeria, Burkina Faso, Equatorial Guinea, Sudan
KUNDI F: Ivory Coast, Cameroon, Gabon, Msumbiji





# FADLU AJIWEKA SAWA SIMBA

NA ELLY SARONGO

**AMEJIPATA! Unaweza kusema kwa Kocha wa Simba, Fadlu Davids raia wa Afrika Kusini kwa kuonesha kandanda safi ndani ya kikosi hicho kilichofuzu Robo Fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF CC) msimu huu**

Katika dakika 270 sawa na mechi tatu za mwisho kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Fadlu ameonyesha kujipata kutokana na namna ya upangaji wa kikosi chake cha kwanza kilichompa heshima kubwa.

Mechi hizo tatu zilizochezwa ndani ya siku 14, ziliipa Simba pointi zilizoivusha kwenda robo fainali ikiwa ni mara ya sita inafanya hivyo kwenye michuano ya CAF kati ya misimu saba kuanzia 2018/2019.

Ndani ya siku hizo ambazo Simba imecheza mechi ngumu katika mataifa matatu tofauti, Tunisia dhidi ya CS Sfaxien, Angola dhidi ya Bravos do Maquis na nyumbani Tanzania dhidi ya CS Constantine, ikikusanya pointi saba kwa kushinda mechi mbili na sare moja.

Haijapoteza mchezo wowote, huku ikifunga mabao manne na kuruhusu moja ikiwa haijaruhusu wavu wake kuguswa (clean sheet) mara mbili, huku ikimaliza kinara wa Kundi A.

Msauzi huyo ni wazi kile ambacho alikuwa akikitengeneza kwa miezi mitano tangu akabidhiwe kikosi hicho sasa ni kama amekipata na anatamba nacho.

Katika michezo hiyo tatu mfululizo, kikosi chake cha kwanza kilikuwa hivi; Moussa Camara, Shomary Kapombe, Mohammed Hussein 'Tshabalala', Che Malone Fondoh, Abdulrazack Hamza, Yusuph Kagoma, Elie Mpanzu, Fabrice Ngoma, Leonel Ateba, Jean Charles Ahoua na Kibu Denis.

Simba imeruhusu bao moja tu ambalo ilikuwa Januari 12, mwaka huu wakiwa Angola ambako walitoa sare ya bao 1-1 na ilikuwa ni baada ya Che Malone kufanya makosa.

Nyavu zao hazikuguswa wakiwa nyumbani, Januari 19, mwaka huu dhidi ya Constantine na hata walipokuwa ugenini pia, Januari 5 huko Tunisia dhidi ya CS Sfaxien.

# AZIZ KI ANAKAMATIKA HAPA

NA MWANDISHI WETU



**KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Aziz Ki chaguo la kwanza la Kocha Mkuu, Sead Ramovic ujanja wake upo kwenye mguu wake wa kushoto ambao umekuwa na mashuti yenye nguvu kitaifa na kimataifa.**

Ki anaingia kwenye rekodi ya nyota aliyepiga mashuti mengi katika mechi za hatua ya makundi huku mchezo dhidi ya Al Hilal ukitajwa kuwa ni mchezo aliocheza katika ubora wa hali ya juu ugenini.

Rekodi zinaonyesha kuwa kwenye mchezo dhidi ya Al Hilal Ki alipiga jumla ya mashuti matano ambayo yalilenga lango huku moja likiwa ni bao la mapema kabisa dakika ya 7 likiwapa pointi tatu Yanga ugenini.

Ikumbukwe kwamba Al Hilal mchezo wao kupoteza katika hatua ya makundi ilikuwa mbele ya Yanga iliyokuwa ugenini na mchezo wa pili ilipoteza dhidi ya TP Mazembe.

Ki kwenye Ligi Kuu Bara amefunga mabao mawili kama ilivyokuwa kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, ana kazi ya kutetea kiatu cha ufungaji bora ndani ya ligi namba nne kwa ubora.

Msimu wa 2023/24 Aziz Ki alifunga mabao 21 katika hayo alifunga hat trick mbili na alitoa pasi 8 za mabao kwenye mechi 27 ambazo alipata nafasi ya kucheza mchezaji bora wa msimu uliopita.

Msimu wa 2024/25 Ki amecheza mechi 15 akitoa pasi nne za mabao huku akifunga mabao mawili kwenye dakika 1,084 alizocheza huku ujanja wake ikiwa ni mguu wa kushoto ambapo kafunga mabao mawili na yote kwa mapigo ya penalti kumbuka kwamba alikosa penalty moja kwenye mchezo dhidi ya Tabora United.

